HelpAge International
age helps

# Sheria Ya Ndoa, 1971

## Kitini cha Wazee washauri vijijini



BMZ Federal Ministry for Economic Cooperation and Development

HelpAge Deutschland
Alter ist Zukunft

## UTANGULIZI:

Kitini hiki cha Wazee washauri kimetengenezwa kama sehemu ya mradi wa miaka mitatu wa ''Kulinda na kuwaenzi wanawake wazee na kuwawezesha kijamii na kiutamaduni nchini Tanzania''. Mradi huu unalenga kuboresha haki za Wazee (hasa Wazee wanawake) kwa kuwawezesha kupitia shughuli mbali mbali ikiwa ni pamoja na utoaji wa ushauri, kusikiliza malalamiko, na kutoa ushauri nasaha na maelekezo yenye misingi ya kisheria pale inapobidi.

Mradi huu utatekelezwa na shirika la Magu Poverty Eradication Centre (MAPERECE) katika kata nne za Wilaya ya Magu na Kwimba; na Shirika la Saidia Wazee Karagwe (SAWAKA) kwenye kata nne za Wilaya ya Karagwe na Kyerwa. Pia mradi huu unatekeleza mojawapo ya vipaumbele vya Shirika la HelpAge International vya kuwawezesha Wazee wanawake na wanaume kupinga ubaguzi kiumri na kudai haki zao.

Kitini hiki kimetengenezwa ili kitumiwe na watu wenye umri mkubwa na kimeandikwa kwa lugha rahisi ili kuwezesha kuwepo kwa mijadala kati ya Wazee washauri waliopata mafunzo na Wazee watakaohitaji msaada wa kisheria. Maelezo yaliyomo katika kitini hiki yameandikwa kutoka katika Sheria ya ndoa namba 5, (1971) kwa vile sehemu kubwa ya sheria hizi zinahusu masuala ambayo ni ya msingi kwa watu wa aina zote.

Watumiaji wa kitini hiki hasa wanatarajiwa kuwa ni Wazee washauri waliopata mafunzo pamoja na Wazee wengine kwa ujumla. Juhudi za makusudi zimefanyika kuhakikisha kuwa maandishi haya na lugha iliyotumika ni rafiki na imezingatia umri, jinsi, maoni, imani na viwango vya elimu na kwa watu wanaoishi vijijini. Lengo kuu la kitini hiki ni kuwapatia Wazee taarifa rahisi na sahihi za kuwawezesha kutambua masuala yanayoweza kusuluhishwa kwa amani  kwa kutumia mbinu za kienyeji na yale yanayohitaji msaada wa kitaalamu wa kisheria. Kwa hali yoyote ile kitini hiki hakilengi kuwafanya Wazee washauri kudai kuwa wao ni wananasheria ama mawakili, na kwa vyovyote vile hakikutengenezwa kuchukua nafasi ya shughuli za wanasheria ama mawakili waliosomea taaluma hiyo. Kitini kinalenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa rahisi na sahihi ili watu wafanye maamuzi ya busara juu ya hatua za kuchukua, na kuepuka migogoro ya muda mrefu na isiyo ya lazima wakati mawazo yaliyo kwenye kitini hiki yangeweza kutoa mwongozo. Tunaamini kuwa taarifa zilizo kwenye kitini hiki zitakuwa na manufaa kwa Wazee na wanajamii wengine wanaohitaji taarifa kuhusu sheria ya ndoa.

## KUHUSU SISI

HelpAge International ni mtandao wa kimataifa wenye njozi ya kuwa na dunia ambamo Wazee wataishi maisha yenye hadhi, afya na nguvu. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa wazee katika nchi ya Tanzania wanapata fursa sawa ya kutumia rasilimali na huduma kama ilivyobainishwa kwenye sera mbali mbali na mifumo ya sheria kwa kuingiza masuala ya Wazee katika mipango ya maendeleo ya nchi hii, na kuondoa umaskini unaowaathiri Wazee na wategemezi wao.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa anuani ifuatayo;
HelpAge International Tanzania
134 Migombani Street
Regent Estate, Mikocheni
P. O. Box 9846
Dar es Salaam
Tanzania
Email: haitz@helpagetz.org

Magu Poverty Eradication Centre
P. O. Box 333
Magu
Tanzania
Email: maperece@hotmail.com

Saidia Wazee Karagwe
P.O.Box 21
Karagwe
Tanzania
Email: kasawatakaragwe@yahoo.com

## SHUKRANI

Utenegenezwaji wa kitini hiki umewezeshwa kupitia msaada wa Wizara ya Ushirika wa Uchumi na Maendeleo ya Shirikisho la Ujerumani, HelpAge Germany na HelpAge International.

# YALIYOMO

1.0 Maana ya ndoa ........................................ 2

2.0 Vigezo muhimu ili ndoa kuwa halali kisheria........................................ 1

3.0 Taratibu za kufuata kabla ya kufunga ndoa........................................ 5

4.0 Aina za ndoa ........................................ 5

5.0 Kugeuza ndoa ........................................ 5

6.0 Aina za ufungishaji ndoa ........................................ 6

7.0 Dhana ya ndoa ........................................ 6

8.0 Ndoa batili ........................................ 7

8.1 Sababu zinazoweza kuifanya ndoa iwe batili........................................ 7

9.0 Ndoa batilifu ........................................ 8

9.1 Sababu zinazoifanya ndoa kuwa batilifu ........................................ 8

10.0 Haki na wajibu wa mke na mume katika ndoa ........................................ 9
Kutengana ........................................ 10

11.1 Aina za kutengana ........................................ 11

11.2 Kumalizika kwa kutengana ........................................ 12

12.0 Talaka ........................................ 12

12.1 Sababu za kutoa talaka ........................................ 12

12.2 Taratibu za kufuata katika mashauri ya ndoa ........................................ 15

12.3 Matokeo ya amri ya talaka ........................................ 15

12.3.1 Kugawana mali ........................................ 15

12.3.2 Matunzo baina ya watalaka ........................................ 16

12.3.3 Uangalizi na matunzo ya watoto........................................ 16

## MAANA YA NDOA

Kwa kuwa ndoa ni taasisi ya zamani na chimbuko zima la jamii, ni vema maana halisi ya ndoa kisheria ikajulikana.

Kufuatana na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ambayo inasimamia masuala ya ndoa nchini, ndoa imefafanuliwa kuwa ni:-

*"Muungano wa hiari kati ya mwanamume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao yote".*

## VIGEZO MUHIMU ILI NDOA KUWA HALALI KISHERIA

### i) Muungano uwe wa hiari

Mwanamke na mwanaume wanatakiwa kuwa wameamua kwa hiari yao kuishi pamoja kama mke na mume, pasipo kulazimishwa na wazazi, ndugu au jamaa wengine.

Kinyume cha hivyo ndoa yao itakuwa batili kwani kisheria itakuwa kama vile hakuna ndoa.

### ii) Muungano uwe kati ya Mwanamke na Mwanaume

Sheria ya Ndoa Tanzania inaelekeza kuwa ili ndoa kuwa halali na kutambulika kisheria ni lazima iwe kati ya mtu mke na mtu mume. Hivyo basi ndoa siyo kati ya mwanaume na mwanaume au mwanamke na mwanamke.

Hata iwapo itakuwa ni ya hiari, haitakuwa ndoa halali kwa sababu itawahusisha watu wa jinsi moja.

Katika mataifa yaliyoendelea kwa maendeleo ya sayansi na tekinolojia yamewezesha mtu mume kujibadili kwa njia ya upasuaji na kuwa na viungo vya sehemu za siri vya kike, na mtu mke kuwa na viungo vya sehemu za siri vya kiume.

Hata hivyo kisheria mtu huhesabika mke au mume kulingana na viungo vya sehemu zake za siri alivyozaliwa navyo, siyo alivyopata baada ya kufanyiwa upasuaji.

### iii) Muungano ukusudiwe kuwa wa kudumu

Ndoa haitahesabika kuwa ni halali iwapo itafungwa kwa malengo ya kudumu kwa muda tu. Ndoa za mkataba wa muda fulani hazitambuliki kisheria.

Ndoa ikishafungwa haiwezi kufunguliwa kiholela. Mahakama ni chombo pekee chenye mamlaka ya kuvunja ndoa baada ya kuridhika na sababu zilizotolewa.

### iv) Wafunga ndoa wasiwe maharimu

Sheria inakataza ndugu wa damu moja kufunga ndoa. Hawa ni pamoja na mtu kuoa au kuolewa na mzazi wake, mzazi wa mzazi wake, mtoto au mjukuu wake, kaka au dada yake, mama au shangazi au baba wa mjomba wake, shangazi au mjomba wake.

Wengine ambao wamo kwenye kundi la maharimu ni mama wa kambo na mtoto uliye muasili (adoption).

Kisheria ni kosa la jinai kwa mtu kumwingilia maharimu wake hata kama walikubaliana kufanya kitendo hicho.

### v) Wafunga ndoa wawe na umri unaokubalika kisheria

Wakati wa kuoana mwanaume na mwanamke wanatakiwa wawe wametimiza miaka 18. Hata hivyo sheria ya ndoa imeruhusu mwanamke chini ya umri wa miaka 18 lakini sio chini ya miaka 15 kuolewa iwapo atapata idhini toka kwa wazazi (baba au mama) kama baba hayupo, au mlezi kama wazazi wamefariki.

Kwa sababu maalum mahakama inaweza kutoa idhini binti akaolewa akiwa na miaka 14 lakini si chini ya hapo ikiwa kwa mfano ataonekana ana mimba. Pia mahakama inaweza kuruhusu kijana kuoa akiwa chini ya miaka 18 lakini si chini ya miaka 16 kama ataonyesha kuelewa jukumu lake kama mtu mzima.

### vi) Kusiwe na ndoa inayoendelea

Sheria inatambua na kuthamini ndoa ambazo zitakuwa zinaendelea. Mume au mke ambaye yupo kwenye ndoa hawezi kufunga ndoa na mke au mume mwingine ikiwa ndoa yake bado inaendelea. Pingamizi hili laweza lisiwepo kama ni ndoa ya wake wengi.

### vii)Kusiwe na kipingamizi cha ndoa

Ndoa zote hutanguliwa na matangazo ya ndoa hizo kwenye ofisi, taasisi au madhehebu yanayohusika siku zisizopungua 21 kabla ya siku ya kufunga ndoa. Lengo la matangazo hayo huwa ni kutoa nafasi kwa watu wenye pingamizi la ndoa husika kulitoa kwenye sehemu zinazohusika.

Ndoa haitakuwa halali kisheria iwapo imewekewa kipingamizi cha ndoa kilichokubaliwa na mahakama au baraza la usuluhishi.

### viii) Mamlaka ya mfungisha ndoa.

Kuna watu ambao kwa nyadhifa zao wamepewa mamlaka ya kufungisha ndoa. Iwapo wanandoa watafungishwa ndoa na mtu ambaye wanafahamu kuwa hana mamlaka ya kufanya hivyo, basi ndoa yao itakuwa batili.

### ix) Kuwepo kwa wafunga ndoa

Kama ndoa itafungwa bila wafunga ndoa wote wawili kuwepo, ndoa hiyo haitatambulika kisheria. Hata hivyo sheria inaruhusu ndoa kufungwa ikiwa mmoja wa wafunga ndoa hayupo lakini amewakilishwa na mtu ambaye alikuwepo wakati mfunga ndoa ambaye hayupo, alipotoa ridhaa yake ya kuoa au kuolewa.

### x) Mashahidi wa ndoa

Ili ndoa itambuliwe kisheria ni lazima ishuhudiwe na mashahidi wasiopungua wawili ambao wanaruhusiwa kisheria, yaani wenye umri usiopungua miaka 18 na wanaofahamu kinachosemwa na kutendeka wakati wa kufunga ndoa.

### xi) Kutokuwa katika Eda

Mwanamke ambaye ndoa yake ilifungwa kiislamu hutakiwa kuwa katika Eda, ambacho ni kipindi cha miezi minne na siku kumi tangu pale anapoachika au kufiwa na mumewe.

Mwanamke wa aina hiyo akiolewa wakati kipindi chake cha Eda hakijaisha basi ndoa hiyo itakuwa ni batili.

## TARATIBU ZA KUFUATA KABLA YA KUFUNGA NDOA

Kabla ya kufunga ndoa inatakiwa mambo yafuatayo yazingatiwe:

- Wanaotarajia kufunga ndoa wanawajibika kutoa taarifa ya nia ya kufunga ndoa kwa mfungisha ndoa si chini ya siku 21 kabla ya siku ya kufunga ndoa, wakieleza taarifa zao muhimu.

- Baada ya kupokea taarifa ya nia ya kufunga ndoa kutoka kwa wanandoa watarajiwa, mfungisha ndoa atawajibika kutangaza nia hii ya kufunga ndoa. Hatua hii inalenga kuwawezesha wenye kipingamizi na ndoa hiyo kutoa taarifa.

## AINA ZA NDOA

Kuna aina mbili za ndoa:

### i) Ndoa ya mke mmoja

Mtu aliyefunga ndoa hii hawezi kufunga ndoa na mtu mwingine hadi pale ambapo mahakama itakuwa imeridhika na sababu zilizotolewa ili kuivunja ndoa ya awali. Ndoa nyingi za kikristo zinachukuliwa kuwa ni ndoa za mke mmoja.

### ii) Ndoa ya zaidi ya mke mmoja

Huu ni muungano kati ya mume mmoja na wake wengi. Kisheria ndoa zinazofungwa kwa utaratibu huu ni zile za kimila na kiislamu.

Ndoa inayofungwa kiserikali pia yaweza kuwa ya wake wengi, mradi tu wahusika wadhihirishe nia yao ya kufunga ndoa ya wake wengi wakati wanapofunga ndoa.

## KUGEUZA NDOA

Kugeuza ndoa ni hatua ya wanandoa kuamua kubadili ndoa yao, kwa mfano kutoka ndoa ya mke mmoja na kuifanya ya wake wengi.

Mtu haruhusiwi kugeuza ndoa bila kufuata taratibu za kisheria. Wanandoa wanaokusudia kugeuza ndoa yao, kwa hiari yao, wanatakiwa kutoa tamko la maandishi lenye sahihi zao na kushuhudiwa na Hakimu au Jaji.

Hata hivyo mageuzo hayo hayahusu ndoa zote zilizofungwa kikristo.

## AINA ZA UFUNGAJI NDOA

Sheria inatambua aina tatu za ufungaji wa ndoa:

i) Ndoa ya kiserikali

ii) Ndoa ya kidini

iii) Ndoa ya kimila

### I) NDOA YA KISERIKALI

Ndoa hii hufungwa mbele ya Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye Msajili wa ndoa. Ndoa hii hufungwa kwa kufuata utaratibu wa kisheria ikiwa ni pamoja na kufungiwa sehemu iliyo wazi ili ishuhudiwe na watu wenye uwezo wa kufanya hivyo.

### II) NDOA YA KIDINI

Ndoa hizi hufungwa kwa mujibu wa taratibu na masharti ya dini inayohusika. Ikiwa wanandoa watakuwa wakristo kwa vyovyote vile ndoa yao itakuwa ya mke mmoja. Kama wanandoa ni waislamu wanaruhusiwa kufunga ndoa ya wake wengi wasiozidi wanne.

### III) NDOA YA KIMILA

Ndoa hizi hufungishwa na mtu yeyote anayetambulika katika eneo hilo kuwa ana uwezo wa kimila wa kufungisha ndoa. Mtu huyu aweza kuwa mzee katika eneo hilo.

Inatakiwa Katibu Tarafa apewe taarifa kuhusu ndoa hizi kwani ndiye msajiri wa ndoa zilizofungwa kimila.

Ndoa za kimila huchukuliwa kuwa ni ndoa za wake wengi.

### UFUNGAJI NDOA NJE YA NCHI

Waziri wa sheria anayo mamlaka ya kuteua baadhi ya maofisa ubalozi kuwa wasajili wa ndoa. Utaratibu unaotumika ni ule wa kufungisha ndoa za kiserikali.

### DHANA YA NDOA

Mwanamke na mwanamume wakiishi pamoja huweza kuchukuliwa kuwa ni mke na mume mbele ya sheria japo hawajafunga ndoa, ikiwa itathibitika kuwa:

- Mwanamume na mwanamke wameishi pamoja kwa muda wa miaka miwili au zaidi mfululizo.

- Umma unaowazunguka unawachukulia na kuwapa hadhi ya mke na mume.
- Watu hao walikuwa na uwezo wa kuwa mke na mume wakati walipoanza kuishi pamoja (umri uliokubalika kisheria).
- Kati yao au wote wawili hakuna aliye na ndoa inayoendelea.

## NDOA BATILI

Ndoa batili maana yake ni ndoa tupu au isiyokuwa na nguvu. Kwa maana nyingine ni Ndoa ambayo siyo halali kisheria. Ndoa hii huwa kama vile haikupata kufungwa (ni shughuli inayofikiriwa kuwa ni kufunga ndoa). Hatma ya Ndoa ya namna hii hufutwa na Mahakama.

Kuvunjwa kwa ndoa hizi hakuwalazimu wanandoa kwenda mahakamani, ila mahakama yaweza kutoa tamko kwa watu wote kuwa iliyokuwa ikidhaniwa kuwa ni ndoa, siyo ndoa.

Kama kutakuwa na watoto waliozaliwa katika ndoa hii watatunzwa na mzazi atakayeteuliwa.

### SABABU ZINAZOWEZA KUIFANYA NDOA IWE BATILI

- Umri wa wafunga ndoa kuwa chini ya ule unaokubalika kisheria.
- Maharimu.
- Kuwepo kwa ndoa inayoendelea.
- Kuwepo kwa pingamizi la ndoa.
- Kulazimishwa kwa wanandoa kufunga ndoa.
- Kutokuwepo kwa wafunga ndoa wakati wa ndoa.
- Mfungisha ndoa kutokuwa na mamlaka ya kufungisha ndoa.
- Kutokuwepo kwa mashahidi wawili wa ndoa wanaokubalika.
- Ndoa ya muda.
- Mke muislamu kuolewa akiwa katika Eda.

# NDOA BATILIFU

Ndoa batilifu ni ndoa halali kama ndoa nyingine isipokuwa inakuwa na kasoro fulani zinazotoa uhalali kwa mwanandoa yoyote anayekerwa na kasoro hizo kuiomba mahakama kuifuta ndoa husika. Hii ni ndoa halali hadi hapo mmoja wa wanandoa atakapochukua hatua ya kuiomba mahakama kutoa amri ya kuifuta kutokana na sababu au kasoro zilizojitokeza baada ya kufungwa. Vinginevyo ndoa hiyo itaendelea kuwa halali kisheria.

Hivyo wanandoa wana haki na wajibu kama wanandoa wengine na watoto waliozaliwa ni halali kisheria.

Ikiwa mfunga ndoa anayedhurika na kasoro zilizopo hachukui hatua za kuivunja, basi ndoa hiyo itadumu kama ndoa nyingine.

## SABABU ZINAZOIFANYA NDOA KUWA BATILIFU

### Kushindwa kuitimiliza ndoa

Lengo la kufunga ndoa ni pamoja na kuwepo kwa tendo la ndoa. Ndoa itakuwa batilifu ikiwa mmoja wa wafunga ndoa anashindwa kuitimiliza ndoa yake.

Hali hii yaweza kusababishwa na mume kuwa hanithi au kwa mwanamke kuwa na hali ambayo inamfanya asiweze kuingiliwa na mwanamume kwa sababu za kimaumbile.

*Kuna mambo muhimu ya kuzingatia katika suala hili:*

- Ni lazima ithibitishwe na daktari kuwa hali hiyo haitibiki.
- Lazima mwanandoa anayelalamika athibitishe kuwa wakati wa kufunga ndoa hakujua kuwa mwenzie alikuwa hawezi kuitimiliza ndoa.
- Iwapo kasoro hizo zitatokea baada ya kufunga ndoa (baada ya kuitimiliza ndoa) hiyo haitakuwa sababu ya kuifanya ndoa iwe batilifu.

### Maradhi ya zinaa

Ikiwa itathibitika kuwa mmoja wa wanandoa alikwisha ambukizwa magonjwa ya zinaa kabla ya ndoa.

### Mimba ya mwanamume mwingine

Ikiwa itathibitika kuwa wakati wa ndoa tayari mwanamke alikuwa na ujauzito wa mwanaume mwingine.

### Wazimu au kifafa cha vipindi

Ikiwa mmoja wa wanandoa atakuwa anaugua ugonjwa wa kifafa au wazimu unaojirudia, na wakati wa ndoa mwenzake hakujua kuwa anao ugonjwa huo.

### Kukataa kwa makusudi kuitimiliza ndoa

Ikiwa baada ya ndoa mmoja wa wanandoa atakataa kwa makusudi kutimiliza ndoa – yaani kufanya tendo la ndoa.

Hii itakuwa na uzito itakapothibitishwa kuwa yule anayekataa hana sababu za kukataa na yule anayekataliwa amefanya kila linalowezakana kumshauri mwenzie wafanye tendo hilo bila mafanikio.

## HAKI NA WAJIBU WA MKE NA MUME KATIKA NDOA

### i) Kutunzana

Ni wajibu wa wanandoa kutunzana kulingana na majukumu yao waliyopeana. Kwa kawaida mume ndiye hufanya kazi ya kutafuta pesa, hivyo ana wajibu wa kumtunza mke au wake zake kwa kuwapatia mahitaji muhimu kama malazi, chakula, matibabu kulingana na uwezo alionao.

Mke au wake nao wana wajibu wa kumtunza mume wao kwa kumpatia mahitaji yote muhimu ikiwa mume kutokana na sababu za maradhi au nyingine za maana ameshindwa kufanya shughuli za kujikimu kimaisha.

Iwapo mume ana mke zaidi ya mmoja ana wajibu wa kuwatunza wote bila upendeleo. Pia mume ana wajibu wa kuwatunza watoto wote waliozaliwa ndani ya ndoa.

### ii) Kumiliki mali

Mke, kama alivyo mume, ana haki ya kumiliki mali aliyoipata kabla ya ndoa na hata wakati wa ndoa kama ameipata kwa fedha zake mwenyewe. Pia mke au mume ana haki ya kuingia mikataba, kufungua madai dhidi ya wadeni wake, kudaiwa, kununua mali au kuiuza.

Ndoa haibadilishi haki ya kumiliki mali kati ya mke na mume, ingawa wanandoa wanaweza kukubaliana kuwa mali walizokuwa nazo kabla ya ndoa ziwe za pamoja.

### iii) Mali iliyopatikana wakati wa ndoa

Mali ya mke au mume iliyopatikana kutokana na jasho lao wote wawili wakati wa ndoa ni mali yao kwa pamoja hata kama juhudi zao au jasho lao katika kupata mali hizi si sawa sawa.

Kuna dhana inayokanushika kuwa, endapo mali itakuwa imeandikishwa kwa jina la mmoja wao basi ni mali yake. Hivyo ni wajibu wa mdai kudhibitisha kuwa pamoja na kuandikishwa kwa jina la mmoja wao ni mali ya pamoja.

### iv) Haki ya kuishi katika nyumba ya ndoa

Nyumba ya ndoa ni nyumba ambayo mume na mke wanaishi wakati wa ndoa. Kama wanandoa wana nyumba nyingi ni nyumba moja tu ndiyo inachukuliwa kama nyumba ya ndoa.

Nyumba ya ndoa haiwezi kuuzwa, kuwekwa rehani au kutolewa kwa mtu mwingine kama zawadi bila makubaliano ya wanandoa wote wawili.

### v) Mke kukopa kwa dhamana ya mume wake

Kawaida ni haki ya mume kumtunza mkewe na watoto. Ikiwa mume atasafiri kwa muda mrefu bila kuacha fedha za kutosha, au akimtoroka mke; mke ana haki ya kukopa fedha kwa jina la mumewe, kuweka rehani mali ya mumewe ili aweze kununua mahitaji ya muhimu kwa ajili yake na watoto wake.

Hata hivyo ni lazima mke atumie haki hiyo kununulia mahitaji yale tu ambayo mume akiwepo huwa na uwezo wa kuyanunua. Pia haki hii haitakuwepo ikithibitika kuwa mke alikuwa na pato la kutosha kuwalisha wanae na yeye mwenyewe bila msaada wa mume wake.

### vi) Heshima

Bila kujali kwenda kinyume cha mila yoyote, hakuna haki yoyote ya mke kumpiga mume au mume kumpiga mke. Kufanya hivyo ni kosa la jinai kama ambavyo umempiga mtu yeyote mwingine.

### vii) Haki ya mjane kuishi anapotaka

Mjane ana uhuru wa kuishi mahali popote anapopenda baada ya mumewe kufariki. Anao uhuru wa kuolewa au kutoolewa tena.

## KUTENGANA

Kutengana maana yake ni utaratibu wa mke na mume kuishi mbali mbali kwa mapatano kati yao au kwa amri ya mahakama ili mume, mke au wote wawili wapate nafasi ya 'kupumua' na kutafakari kiini cha matatizo ya ndoa yao na ikiwezekana kujirudi na kurudiana.

Kutengana siyo talaka ila ndoa inakuwa na misukosuko ambayo haijafikia kiwango cha

kutorekebika na matumaini ya kurudiana yanakuwepo.

Wakati wa kutengana wanandoa wanakuwa wameondoleana majukumu ya kila mmoja kumhudumia mwenziye kwa vile wanakuwa wanaishi mbali mbali.

Wakati wa kutengana mume au mke hatahesabika kuwa ni mtoro ingawa atakuwa anaishi mbali na mwenziye.

Hata hivyo kutengana kukiendelea kwa muda wa miaka mitatu au zaidi hiyo yaweza kuwa sababu ya kudai talaka na mahakama inaweza kuivunja ndoa husika.

## AINA ZA KUTENGANA

Kuna aina mbili za kutengana:

i) Kutengana kwa makubaliano.

ii) Kutengana kwa amri ya mahakama.

### i) Kutengana kwa makubaliano

Kutengana kwa mapatano hutokea pale ambapo wanandoa huamua kwa hiari yao wote wawili kuishi mbali mbali.

Makubaliano haya hufanywa kwa maandishi na mara nyingi huhusisha vipengele ambavyo hutakiwa kuzingatiwa. Walio wengi huwekeana masharti yafuatayo:

- Kutobughudhiana - hii ni pamoja na kutotembea nje ya ndoa au mwanandoa mmoja kumfuata fuata mwenzie mahali anapoishi bila sababu ya maana au kutaka kufanya naye tendo la ndoa.

- Utaratibu wa matunzo ya watoto ambao hautawaathiri watoto wao. Mwanandoa ana haki ya kuwatembelea watoto wanaotunzwa kwa mwanandoa mwenzie, bila pingamizi lolote.

### ii) Kutengana kwa amri ya mahakama

Mahakama inaweza kutoa amri ya kutengana kwa wanandoa kwa ombi la mmoja wao au kwa kuona hali ya mwanandoa mmojawapo ipo hatarini.

Sababu zinazosababisha kutolewa kwa amri ya kutengana ni zile zile zinazowafanya wanandoa kukubali kuishi mbali mbali.

Pamoja na kutoa amri ya kutengana, mahakama pia inaweza kutoa amri kuhusu matunzo ya watoto.

## KUMALIZIKA KWA KUTENGANA

Kutengana humalizika wakati wowote wanandoa wanapokubaliana kurudiana kama walivyokuwa wamekubaliana kutengana. Kama kutengana kulitokana na amri ya mahakama, basi kutengana humalizika pale mmoja wa wanandoa ambaye alikuwa amepeleka ombi la kutengana mahakamani ataiomba mahakama kutengua amri hiyo ya kutengana.

Pia mahakama inaweza kuifuta amri ya kutengana ikiwa itathibitika kuwa amri hiyo ilitokana na maneno ya kupotosha yaliyotolewa na mmoja wa wanandoa.

Amri ya kurudiana inapotolewa wanandoa wanatakiwa kurudiana na kuanza kuishi pamoja mara moja. Ikiwa mwanandoa mmojawapo atakaidi, basi atahesabika kuwa ni mtoro kuanzia siku ile alipokataa kurudiana na mwenzie.

## TALAKA

Talaka ni utaratibu rasmi wa sheria wa kuvunja ndoa halali. Ingawa dhamira ya sheria ya ndoa ni ndoa kudumu katika kipindi chote cha maisha ya wanandoa vilevile imetambua katika mazingira fulani upo uwezekano wa ndoa kuwa katika migogoro mikubwa na kushindwa kuendelea. Hata hivyo, mahakama ndicho chombo pekee chenye mamlaka ya kisheria kutoa talaka hapa nchini.

Mahakama hutoa talaka pale tu itakapothibitika kuwa jitihada zote za kuiokoa ndoa husika zimeshindikana.

## SABABU ZA KUTOA TALAKA

Mahakama hutoa talaka ikiwa imeridhika kuwa ndoa imevunjika kiasi ambacho haiwezi kurekebishika tena.

Sheria ya ndoa imeainisha sababu zinazoweza kusababisha ndoa kuvunjika na talaka kutolewa mahakamani ambazo ni pamoja na:

### Ugoni

Hiki ni kitendo cha kufanya tendo la ndoa kwa hiari baina ya mtu aliyeoa au kuolewa na mtu mwingine ambaye siyo mke wake au mume wake. Mtu atahesabika kuwa amefanya tendo la ugoni ikiwa hakulazimishwa au alihiari kufanya tendo hilo.

Ugoni utahesabika umetendeka ikiwa itathibitika kuwa kitendo cha kujamiiana kimetendeka.

Angalizo: Ushahidi wa ugoni huwa ni mgumu sana kuthibitika kwa sababu mambo ya ugoni hufanyika kwa siri sana.

Hata hivyo kuna mambo yanayoashiria kuwa ugoni ulifanyika, mfano mke aliyeolewa na mume aliye safari kwa muda mrefu akionekana na mimba, au kwa mwanandoa mmojawapo kuambukizwa magonjwa ya zinaa na ambaye si mwenzi wake wa ndoa.

Inapotokea mwanandoa akauona ugoni wa mwenzi wake wa ndoa na akaamua kuufumbia macho, basi mahakama haitakubali kuwa ni sababu ya kudai talaka.

Pia ili ugoni kuwa sababu ya kuvunja ndoa ni lazima ugoni huu uwe umefanyika zaidi ya mara moja. Lakini hii hutegemea zaidi mazingira ambayo kitendo hicho kimefanyika.

Mfano: *Mume au mke akiwa amesafiri halafu akute mkewe au mumewe amemwingiza mwanamke au mwanamume mwingine chumbani kwao. Kitendo hiki kinauma sana na kinaweza kuwa sababu ya kutosha kusababisha kuvunjika kwa ndoa.*

### Ukatili

Ukatili ni tabia ya makusudi ambayo inasababisha maumivu ya mwili na msongo wa akili au kuleta hofu inayosababishwa na kuwepo kwa hatari kama hiyo.

Ukatili siyo tu kumpiga mwenzi wa ndoa. Ni pamoja na matendo ya makusudi ya kusononesha, kujihisi mnyonge au kuwa na mawazo mengi yanayomfanya mmoja kukosa raha.

Mfano hali ya ulevi wa kupindukia au kumzulia mwenzi wa ndoa mambo ambayo hajapata kuyatenda.

### Kulawiti

Kulawiti ni kufanya mapenzi kupitia njia ya haja kubwa. Ikiwa mwanandoa anayelalamika atathibitisha kuwa mwenzi wa ndoa alimtaka wafanye kitendo hicho, huo utakuwa ni ushahidi wa kuombea talaka.
Angalizo: Kitendo cha kulawiti ni kibaya sana, ni kinyume cha maadili na ni kosa la jinai.

### Kuzembea wajibu kwa makusudi

Hali hii huwa ni pamoja na kwa mfano mume kutompatia matunzo ya kutosha mke wake kulingana na kipato chake kwa sababu ya ulevi. Au mke anayefanya kazi kuchelewa sana kurudi nyumbani kwa makusudi, akakosa kuwaandalia watoto chakula, akawa hamtunzi mumewe n.k.

## Utoro

Mume anapoamua kuhama katika nyumba ya ndoa na kwenda kuishi mahali pengine bila sababu ya kuridhisha huo huitwa utoro. Kwa mke huwa ni tofauti kidogo.

Kama mke ataamua kuondoka kwa ajili ya ukatili wa mume, basi mume huwa ndiye huhesabiwa mtoro, ambapo kisheria huitwa utoro wa hila.

## Kutengana kwa zaidi ya miaka 3

Hali ya kutengana kwa wanandoa ikizidi kipindi cha miaka mitatu inaweza kuwa sababu ya kuomba kuvunjwa kwa ndoa.

## Kifungo

Ikiwa mwanandoa atafungwa kwa kipindi cha miaka isiyopungua mitano, basi huo unaweza kuwa ni ushahidi wa kuivunja ndoa. Hata hivyo hii ni ridhaa ya mwanandoa aliyeachwa kuona kama ataweza kuvumilia kwa muda huo kwa kuzingatia kosa alilofungwa nalo mwanandoa mwenzake.

## Kichaa kisichopona

Ikiwa mwanandoa ataugua maradhi ya akili ambayo madaktari (mmoja wao akiwa ni bingwa wa magonjwa ya akili) watathibitisha kuwa maradhi hayo ya akili hayawezi kupona, basi huo ni ushahidi wa kuivunja hiyo ndoa.

## Dhana ya kifo

Hii ni kudhania kuwa mtu fulani amekufa, hali ambayo hutokea ikiwa mume au mke ametoweka kwa muda mrefu na hajulikani alipo na juhudi za kupata habari zake hazikufanikiwa kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.

Mahakama hutoa tangazo kuwa fulani amekufa baada ya kuwasilishwa ombi mahakamani na mume au mke anayedhani mwenziye amefariki.

## Tofauti ya itikadi au dini

Katika mfumo wa vyama vingi, tofauti ya itikadi kati ya wanandoa huweza kusababisha ukosefu wa amani na kusababisha kuvunjika kwa ndoa.

Pia ni rahisi ndoa kuingia kwenye migogoro na hata kuvunjika hasa pale Wanandoa wanapokuwa ni waumini wa dini tofauti mfano Mkristo na Muislamu au Mkristo na Mhindu au kinyume chake. Na migogoro hujitokeza pale mmoja wa wanandoa anapomlazimisha mwenzake kubadili dini yake.

## TARATIBU ZA KUFUATA KATIKA MASHAURI YA NDOA (KUOMBA TALAKA/KUVUNJA NDOA)

Angalizo: Mahakama haikubali kusikiliza shauri ambalo mlalamikaji anadai talaka ikiwa ndoa haijadumu miaka miwili, isipokuwa kama itathibitika kuwa mlalamikaji yumo katika taabu au shida kubwa ambayo hawezi kuendelea kuivumilia.

Migogoro yote inayohusu ndoa lazima ianze kwanza katika mabaraza ya usuluhishi ya ndoa, ambapo kiini cha mgogoro huchunguzwa na kuwasuluhisha wanandoa.

Mabaraza ya usuluhishi ya ndoa yanayo tambulika kisheria ni pamoja na:

- Ofisi za Ustawi wa jamii
- BAKWATA kwa Waislamu
- Baraza la kata la usuluhishi la ndoa n.k.

Inapotokea baraza linashindwa kusuluhisha wahusika, hutoa shahada maalum (Fomu mamba 3) inayothibitisha kuwa baraza limeshindwa kuwasuluhisha wanandoa, na pia hutoa mapendekezo yake kuhusu ndoa husika.

### MATOKEO YA AMRI YA TALAKA

Ndoa huhesabika kuwa imevunjika siku 30 baada ya hukumu yaani talaka kutolewa. Baada ya hapo wanandoa huwa na hadhi mpya kisheria. Kila mmoja huwa na haki ya kuoa au kuolewa tena.

Kwa waislamu wanawake hutakiwa kukaa Eda ya miezi minne na siku kumi kabla ya kuolewa tena.

Angalizo: Ni dhahiri kwamba, ndoa inapovunjika mambo mengi huathirika ikiwa ni pamoja na uangalizi wa mali na matunzo ya watoto. Hali hii huwa ni janga kwa watoto wa waliokuwa wanandoa.

### KUGAWANA MALI

Kama tulivyoona awali, katika ndoa huwa kuna mali ambazo zilipatikana toka kwa wanandoa binafsi na nyingine zilizopatikana kwa juhudi zao za pamoja.

Mali inayogawanywa wakati wa talaka ni ile ambayo:

- Imetokana na kuwepo kwa ndoa. Yaani bila ndoa mali hiyo isingekuwepo.

- Imepatikana wakati wa ndoa.

- Imepatikana kutokana na juhudi za pamoja. Kisheria juhudi za pamoja zilitafsiriwa kuhusisha pia shughuli zote za nyumbani ambazo mke huzifanya akiwa nyumbani.

Shughuli hizi siyo lazima ziwe za kuthamanishwa na fedha, bali umuhimu na muda wa shughuli hizo huchangia sehemu kubwa katika upatikanaji wa mali ya pamoja.

Kazi hizi ni pamoja na kutunza watoto, kuandaa chakula, kutunza nyumba n.k. Yaani kazi zote ambazo humwezesha mume kufanya kazi zake vizuri zaidi kwa kutokuwa na wasiwasi juu ya hali ya watoto wake na nyumba/ mali zake.

## MATUNZO BAINA YA WATALIKI

Mahakama pia inaweza kutoa amri ya matunzo kwa waliokuwa wanandoa, hasa mke. Sheria inatambua matatizo ambayo waliokuwa wanandoa huyapata baada ya talaka kama vile upweke na majukumu yanayofuata ambayo huwa si jambo rahisi kwa yule asiye na uwezo. Hivyo yule mwenye uwezo anatakiwa kuendelea kumtunza aliyekuwa mwenzake hata baada ya kuachana kwa muda ambao mahakama itaona unafaa.

Suala la matunzo hutolewa kwa ridhaa ya mahakama lakini si suala ambalo linaweza kudaiwa mahakamani kama haki kwa yeyote asiyekuwa na uwezo.

## UANGALIZI NA UTUNZAJI WA WATOTO

Mahakama hutoa amri ya uangalizi wa watoto kama wapo. Uamuzi wa mahakama kuamua iwapo watoto wanafaa kuishi kwa baba au mama yao huzingatia pamoja na mambo mengine:

- **Umri wa watoto**

Mahakama huangalia maslahi ya watoto, kwa maana ya mazingira ambayo yatawawezesha watoto hao kukua na kustawi vema kiafya, kielimu na kimaadili. Hivyo kawaida mahakama hutoa uangalizi wa watoto kwa yule anayeweza kuwaaangalia watoto kwa kuzingatia maslahi ya watoto hao.

Mara nyingi mtoto mwenye umri wa chini ya miaka saba hupewa uangalizi wa mama labda pale itakapothibitishwa kuwa mama huyo hawezi kumtunza mtoto huyo kwa mfano kama mama huyo ana tabia za ulevi uliopindukia, umalaya au uvivu iliokithiri.

Watoto wengine wanaweza kuchagua ni sehemu gani watapenda kuishi.

- **Mazingira ya mzazi anayewachukua**

Kama ilivyodokezwa hapo juu, mahakama huwa makini kuhakikisha kuwa uangalizi wa watoto hautolewi kwa mzazi ambaye mazingira anamoishi au tabia yake mbaya inaweza kuwaathiri watoto kimwili, kiafya, kitabia au kisaikolojia.

Wajibu wa kuwatunza watoto huanzia kwa baba pasipo kuzingatia kama watoto wapo katika uangalizi wa mtu mwingine.

Kama baba atafariki, atakuwa hayupo (mtoro) au uwezo wake ni mdogo, basi mama huchukua jukumu la kuwatunza watoto.

- **Madhara ya talaka kwa wanandoa**

Pamoja na kueleza taratibu za kutoa talaka, inasisitizwa kwamba suala la talaka linapashwa kuwa ni suluhisho la mwisho. Hii ni kwa sababu madhara ya talaka huwa ni kwa wanadoa, watoto, wazazi wa wanandoa pande zote mbili, jamii inayowazunguka na hata taifa. Madhara ya talaka yanaweza kuwa ya aina mbalimbali lakini makubwa ni kama yafuatayo;

i. Kusambaratika kwa mali za wanandoa kwa sababu mali hugawanywa kwa wanandoa wote kulingana na mchango wao.

ii. Watoto kukosa malezi bora na matunzo ya wazazi.

iii. Kujengeka kwa uhasama kati ya familia za wandoa.

iv. Gharama na muda wa kushughulikia madai ya talaka.

Wajibu wa kuwatunza watoto huanzia kwa baba pasipo kuzingatia kama watoto wapo katika uangalizi wa mtu mwingine.

Kama baba atafariki, atakuwa hayupo (mtoro) au uwezo wake ni mdogo, basi mama huchukua jukumu la kuwatunza watoto.

Pamoja na kueleza taratibu za kutoa talaka, inasisitizwa kwamba suala la talaka linapasHwa kuwa ni suluhisho la mwisho. Hii ni kwa sababu madhara ya talaka huwa ni kwa wanadoa, watoto, wazazi wa wanandoa pande zote mbili, jamii inayowazunguka na hata taifa. Madhara ya talaka yanaweza kuwa ya aina mbalimbali lakini makubwa ni kama yafuatayo;

i. Kusambaratika kwa mali za wanandoa kwa sababu mali hugawanywa kwa wanandoa wote kulingana na mchango wao.

ii. Watoto kukosa malezi bora na matunzo ya wazazi.

iii. Kujengeka kwa uhasama kati ya familia za wandoa.

iv. Gharama na muda wa kushughulikia madai ya talaka.

HelpAge International
age helps

HelpAge International Tanzania
134 Migombani Street, Regent Estate, Mikocheni
P.O. BOX 9846 Dar es Salaam Tanzania
Tel: +255 22 2774796/2700169
Fax: +255 22 2775894

Email: haitz@helpagetz.org
Website: www.helpage.or

Copyright © HelpAge International 2014
Registered charity no. 28810